BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# MUKHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA YA UMMA (LAAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA 2019/2020 NA 2020/2021

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika kutekeleza majukumu yetu kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha Mukhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma (LAAC) uliolenga kwenye Ripoti tatu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama zifuatazo;

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020
2. Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; na
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Sambamba na kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Toleo la mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako kuwa Kamati ya LAAC haikuweza kuikamilisha kuifanyiwa kazi, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na ufinyu wa muda, hivyo, Kamati inaahidi kuendelea kuikamilisha Ripoti hiyo katika mizunguko ijayo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukurani za dhati kwa Serikali za Mitaa, Mashirika, Taasisi Zinazojitegemea za Serikali na wananchi wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine katika shughuli za Kamati kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii

wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba.

**Mheshimiwa Spika,** tunatoa shukurani za pekee kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati ya LAAC kushiriki katika Mikutano mbali mbali ya Kimataifa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na Kamati nyenzake zenye asili kama hiyo na hatimae Kamati kutoa mapendekezo yake kwa Afisi ya Baraza kwa yale maeneo ambayo imehisi kuna haja ya kuyafanyia marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** tunatoa shukurani pia kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kuipatia mafunzo Kamati hii ili iweze kutekeleza shughuli zake kwa wepesi na kwa weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Katibu wa Baraza pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya LAAC, Makatibu Kamati pamoja na Maafisa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa umahiri wao wa hali ya juu waliouonesha hadi tunawasilisha Ripoti hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Habib Ali Mohamed - Mwenyekiti;
2. Mhe. Mwaanasha Khamis Juma - Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Mjumbe;
4. Mhe. Haji Shaaban Wazir - Mjumbe;
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe;
6. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe;
7. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu;
8. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu;
9. Ndg. Hamad Akida Hamad - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti;
10. Ndg. Shehe Abdallah Ali - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti;
11. Ndg. Maryam Alhaj Juma - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti na
12. Ndg. Abdallah Khamis Omar - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti Pemba.

## 2.0 YALIOBAINIKA KWA KILA RIPOTI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC ilizifanyia kazi Ripoti tatu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za miaka miwili tofauti pamoja na kuzingatia maelekezo ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020. Katika kutekeleza shughuli hiyo, Kamati hii iliyafanyia kazi maeneo matatu kama ifuatavyo:

1. Mapato na Matumizi ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Umma;
2. Ukiukwaji wa taratibu mbali mbali zilizofanywa na Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Umma; na
3. Hali ya Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuyafanyia kazi maeneo hayo baadhi ya mambo yafuatayo kwa ujumla wake yamebainika na maelezo kamili kuhusiana na yaliyobainika ni kama inavyoonekana kwenye Ripoti kuu ya Kamati hii ambayo inapatikana kwenye "tablet" zenu.

**1. Taarifa za Mapato na Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC katika kufuatilia eneo la mapato ya Serikali za Mitaa imebaini kuwa baadhi ya Serikali za Mitaa zimeshindwa kufikia malengo kutokana na vianzio vyao vikuu vya mapato kusimamiwa na Serikali Kuu na matokeo yake vianzio hivyo havikukusanya vyema, lakini pia hicho kidogo kilichopatikana ama wanapatiwa kidogo zaidi na baadhi ya miaka hawapatiwi kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa Serikali za Mitaa ambazo kianzio chake kikuu kinasimamiwa na Serikali Kuu ni Baraza la Mji Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani ambayo yanategemea kianzio kinachotokana na kware.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Baraza la Mji Chake chake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kianzio cha mapato cha kware kilikusanya Tsh. 75,200,000 wakati mwaka wa fedha 2019/2020 kilikusanya Tsh. 15,420,000 tu, ingawa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza lilikadiria kukusanya Tsh. 57,840,000.

**Mheshimiwa Spika,** hiyo ni kasoro kubwa na kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuliangalia upya suala hilo ili Serikali za Mitaa ziweze kupata mapato yake kutokana na vianzio vyake ili tija ya kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa iweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali Kuu kuhakikisha kuwa inazipatia Serikali za Mitaa kwa wakati na kwa asilimia waliokubaliana fedha za mapato yanayosimamiwa na Serikali Kuu kwa niaba ya Serikali za Mitaa ili kuheshimu makubaliano yaliyopo pamoja na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake bila ya usumbufu wowote.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Kamati ya LAAC inashauri kuwekwa mifumo ambayo itasaidia kupatikana kwa uwazi juu ya makusanyo mbali mbli ya Serikali za Mitaa kwani kila mmoja ataweza kujua kiwango kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa Serikali Kuu

baadhi ya wakati huingilia utendaji wa Serikali za Mitaa ambazo zipo kisheria hususan katika eneo la mapato na kutoa maamuzi ambayo hayana tija kwa Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mifano mbali mbali iliyoelezwa Kamati ya LAAC wakati inatekeleza majukumu yake, hata hivyo, tunaomba kuthibitisha kauli yetu hiyo kupitia maamuzi ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Malum za SMZ ya kuwataka Wakurugenzi wote wa Serikali za Mitaa kumtumia Wakala ambae ni Kampuni ya Al jumura katika kukusanya mapato ya minara pamoja na kukusanya deni lililokuwa la muda mrefu katika Kampuni za Minara.

**Mheshimiwa Spika,** maamuzi hayo ya Serikali Kuu hayakuleta tija kwani Kampuni ya Al jumuira haikutekeleza vyema wajibu wake na hatimae Serikali Kuu kuzitaka Serikali za Mitaa kusitisha mkataba na Kampuni hiyo na jukumu la kukusanya mapato ya minara kukabidhiwa Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA).

**Mheshimiwa Spika,** maamuzi yote mawili ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa hayakuzaa matunda kwani Kamati ya LAAC ilielezwa kuwa baada ya shughuli hiyo kusimamiwa na Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar, Serikali za Mitaa hazijapatiwa hata senti moja inayotokana na mapato hayo na endapo zitafuatilia basi majibu wanayopewa ni kuwa wao hawatambuliki kisheria kwa kuwa sio waliofunga mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** mara kadhaa tumekuwa tunazilaumu Serikali za Mitaa kuwa hazitekelezi vyema majukumu yake ikiwemo ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kumbe zina sababu za msingi za kushindwa kutekeleza hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali Kuu kuendelea kusimamia Serikali za Mitaa na sio kuingilia moja kwa moja utendaji wa wao na endapo itabaini kuna tatizo ndani ya Serikali za Mitaa ni vyema wakakaa pamoja na kujadiliana juu ya jambo husika na sio kushushiwa aagizo tu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hoja namba 5.4.2.1 kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) bado zipo Taasisi za Serikali hazikusanyi baadhi ya mapato ingawa mapato hayo yapo Kisheria na Kikanuni kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ya PAC ya Baraza la Tisa la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake makini Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa iliwahi kulibaini tatizo hilo na mnamo tarehe 21 Januari, 2019 aliandaa kikao cha pamoja kilichowajumuisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usarifishaji, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usarifishaji, Mkurugenzi

Mkuu, Mamlaka ya Usafiri Baharini na Mkurugenzi Mkuu wa ZURA.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kikao hicho ilikuwa ni kutaka kujua sababu zinazoipelekea Serikali kutoiruhusu ZMA kukusanya tozo hiyo kwa kuwa pamoja na mambo mengine ZMA ndio taasisi yenye jukumu la kuhifadhi mazingira ya bahari na zipo baadhi ya meli hutokea kuchafua mazingira kwa kudondosha mafuta baharini, lakini pia, suala la kukusanya tozo hiyo lipo kwa mujibu wa kanuni ya 4 ya Kanuni za Tozo zilizotungwa chini ya kifungu cha 491 cha Sheria Namba 5 ya mwaka 2006.

**Mheshimiwa Spika,** hakukuwa na jibu la moja kwa moja kwa upande wa Serikali kuhusiana na suala hilo, isipokuwa kwamba, Serikali iliahidi kulifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa hadi Kamati ya LAAC ilipofanya uchunguzi wake kwa ZMA tarehe 01 Februari, 2023 ilibaini kuwa changamoto hiyo bado haijapata ufumbuzi licha ya kuwa muda mrefu umepita.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC ilishtushwa na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohammed mbele ya Baraza lako tarehe 20 Februari, 2023 alivyokuwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa kuhusiana na ZMA kutokutoza tozo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC ilishtushwa kwa kuwa hatua zote nzuri na muhimu zilizoanza kuchukuliwa na Serikali haikushirikishwa ZMA na ndio maana ZMA iliieleza Kamati hii kuwa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa juu ya suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua hizo nzuri zilizofikia zilizoelezwa na Mheshimiwa Waziri, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuishirikisha ZMA katika kila hatua kwa kuwa suala hilo limo ndani ya Taasisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine Kamati ya LAAC inaishauri Serikali endapo itaendelea kuona kuwa hakuna haja ya ZMA kutoza tozo hiyo na wala hakuna marekebisho yoyote ya Sheria na Kanuni yatakayofanywa basi ni busara kwa Serikali ikafidia tofauti ya fedha iliyopo ili Mamlaka iweze kupata mapato yake kamili kwa mujibu wa Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa zipo baadhi ya Taasisi za Umma ambazo zinaweza kuanzisha vitega uchumi kwa ajili ya kukuza mapato yake kama Taasisi nyengine duniani zenye uasili kama huo zinavyofanya. Mheshimiwa Spika, hapa tunalikusudia Shirika la Magazeti Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** asilimia kubwa ya Mashirika ya Magazeti ulimwenguni huchapisha magazeti yake wenyewe kwa lengo la kuchapisha gazeti kwa gharama nafuu zaidi, lakini pia, Mashirika hayo hujishughulisha kutoa huduma mbali mbali za uchapaji kwa lengo la kukuza mapato ya Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mantiki hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kukifanyia marekebisho kifungu cha 35 cha Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar Namba 12 ya mwaka 2018 ili Shirika la Magazeti liweze kupatiwa mtambo wake na kuweza kutoa huduma kama hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa kwa mujibu wa kifungu hicho cha Sheria ni Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar pekee ndio mwenye jukumu la kuchapa kazi za Serikali ingawa Wakala huyo anaonekana hana uwezo wa kutosha wa kutekeleza hilo, hivyo, ni busara kwa Serikali kutoa fursa na kwa Shirika la Magazeti ili kumpunguzia mzigo Wakala huyo lakini pia, Shirika hili litafanya na kazi za watu binafsi ili kukuza mapato yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati ya LAAC haijaridhika na matumizi mbali mbali yaliyofanywa na Taasisi za Serikali kwa mfano, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** asilimia kubwa ya hoja za Mamlaka hii kwa upande wa Unguja ni kwenda kinyume na vifungu mbali mbali vya Sheria na Kanuni za Ununuzi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kasoro hiyo, Kamati yako ilitaka kujua tatizo linaloikabili Mamlaka hii hususan kwenye eneo la Sheria na Kanuni za Ununuzi ambapo Watendaji wa Mamlaka waliieleza Kamati hii kuwa dosari hizo zimejitokeza kwa kuwa vifaa vinavyonunuliwa na Mamlaka ni vya thamani kubwa na baadhi ya vifaa au huduma wakati mwengine huhitajika haraka. Hivyo, ni vigumu kutumiza masharti ya Sheria na Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haikukubaliana moja kwa moja na maelezo hayo, kwani Sheria na Kanuni hizo zimeeleza kwa kina utaratibu wa kila jambo, hivyo, asilimia kubwa ya hoja za Mamlaka zimebaki kama zilivyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Kamati ya LAAC inaishauri Taasisi inayohusika na Sheria na Kanuni ya Ununuzi kuifanyia marekebisho Sheria na Kanuni hiyo kwa kuwa masharti yaliyowekwa utekelezaji wake unakwaza baadhi ya Taasisi. Hivyo, ni busara ikatungwa Sheria na Kanuni ambayo masharti yake yataziwezasha Taasisi kuitekeleza Sheria hiyo kwa mujibu wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege – Pemba wakati Kamati ya LAAC inafuatilia hoja namba 5.3.1.14 kuhusiana na Hati za Malipo zilizokosekana kwa ukaguzi Tsh. 66,933,487 na hoja namba 5.3.1.15 kuhusiana na Hati za Malipo zenye vielelezo pungufu Tsh. 3,893,165, Watendaji wa Mamlaka waliipatia Kamati baadhi ya Hati za Malipo ambazo kimuonekano zinaonesha kuwa Hati hizo ni za kughushi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC ilisikitishwa sana na jambo hilo na kwa kuwa

Mamlaka hiyo haijawahi kufanya kitendo kama hicho kwa Kamati hii, hivyo, Kamati inaitaka Mamlaka kutokurejea tena kitendo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Umma kuelewa kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe kitendo cha kughushi nyaraka ni kosa na endapo mhusika atashitakiwa basi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Adhabu (Penal Act).

**2. Taasisi za Serikali kutokulipa huduma zinazotolewa na Taasisi Nyengine za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imesikitishwa sana na kitendo cha Taasisi za Serikali kutolipa huduma inayotolewa na Taasisi nyengine ya umma licha ya matumizi ya huduma hizo bajeti yake kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa huduma hizo zinazotolewa ni umeme, maji magazeti, kodi za majengo na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya Taasisi hazilipi huduma hizo kwa kuwa zinaamini kuwa ni kawaida kwa Serikali baada ya muda fulani kulipa fedha hizo kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina ama kuyasamehe madeni yaliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inaelewa kuwa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) zipo chini ya mamlaka ya Afisa Mas'uul, hivyo, Mhasibu Mkuu wa Serikali hawezi kuzikata fedha hizo moja kwa moja na kulipa madeni hayo na hasa ikizingatiwa kuwa hana uhakika kama Taasisi husika ni kweli inadaiwa kiasi hicho cha fedha kinachodaiwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, na kwa kuwa bado Maafisa Mas'uul hawajalichukulia hatua suala hilo, Kamati ya LAAC kwa mara nyengine tena inaishauri Serikali kuanzia mwezi wa Machi, 2023 hadi Juni, 2023 kuzikata Taasisi zake fedha za huduma hizo moja kwa moja kwenye fedha zao za Matumizi Mengineyo (OC) ili Taasisi zinazotoa huduma hizo ziweze kupata mapato hayo kwa lengo la kutekeleza vyema shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC ilitoa ushauri kama huo katika Taarifa yake iliyowasilisha mwaka jana mbele ya Baraza lako Tukufu na kuiomba Serikali kutekelezwa suala hilo kuanzia mwezi wa Machi, 2022. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Taasisi husika na kupelekea madeni hayo kuzidi kuongezeka maradufu kwa mfano, katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu imelezwa kuwa Shirika la Magazeti Pemba hadi mwaka wa fedha 2020/2021 linazidai Taasisi mbali mbali jumla ya Tsh. 48,002,170.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Zanzibar hadi kufikia tarehe 10 Januari, 2023 Shirika hili linazidai Taasisi mbali mbali jumla ya Tsh. 2,310,448,896 na kwa upande wa Tanzania Bara jumla ya Tsh. 554,747,200.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inaishauri tena Serikali kulitekeleza hili kwa kuwa

ushauri kama hao uliwahi kufanyiwa kazi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimae tija ilipatikana, hivyo, hakuna dhambi katika kuiga jambo jema.

**Mheshimiwa Spika,** tunalisisitiza hili kwa kuwa wakati Kamati yako inapofanya kazi zake hupokea sana malalamiko kutoka kwa Taasisi zinazotoa huduma hizo licha ya kuwa baadhi ya Taasisi hupata hoja ya moja kwa moja kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatia kasoro hiyo. Hivyo, ni busara kwa Serikali kulichukulia kwa uzito wake suala hilo ili Taasisi husika ziweze kupata mapato yake pamoja na kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

### 3. Baadhi ya Maagizo ya Serikali kwa Taasisi zake Huchangia Taasisi Kupata Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya maagizo ya Serikali kwa Taasisi zake huchangia Taasisi kupata hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalithibitisha hilo kupitia hoja mbali mbali zilizoibuliwa na Mdhibiti na wakati Kamati inatekeleza shughuli zake majibu ya Taasisi ni kuwa hayo ni maagizo ya Serikali kwa hiyo hawawezi kuyapinga na endapo Taasisi zitatoa maoni au ushauri juu ya jambo husika basi hujibiwa majibu ambayo yanakata tama kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya Taasisi hizo ni Shirika la Bima la Zanzibar ambalo limepata hoja mbili kutokana na maagizo ya Serikali. Hoja zenyewe ni kama zifuatazo:

1. Hoja namba 5.1.2.2 kuhusiana na Shirika la Bima kufanya uwekezaji usiyo na tija wa Tsh. 711,000,000, kati ya fedha hizo jumla ya Tsh. 261,000,000 ni uwekezaji katika Kampuni ya ZAFICO naTsh. 450,000,000 katika Kampuni ya MWANI.
2. Hoja namba 5.1.2.3 kuhusiana na kuendelea kushuka kwa Uwezo wa Shirika wa Kulipa Madai ya Bima(Solvency Margin). Mheshimiwa Spika, katika hoja hii Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Fedha na Mipango ziliitaka Shirika la Bima kulilipa Shirika la Meli deni la Kampuni ya UAP USD 324,166.17 jambo ambalo ni kinyume na masharti ya mkataba baina ya Shirika la Bima na Kampuni ya UAP kwani vyombo viwili hivyo vilifunga Mkataba wa Bima Mtawanyo, hivyo, Shirika la Bima halikupaswa kulipa fedha za upande wa pili.

   Mheshimiwa Spika, kitendo cha Shirika la Bima kulipa fedha hizo kinyume na mkataba kimechangia kwa kiwango kikubwa uwepo wa kuongezeka kwa “solvency margin” katika Shirika kwani Kampuni ya UAP inasuasua katika kulipa deni hilo lakini pia, kimepelekea Shirika la Bima kupata hoja isiyo na msingi kama Serikali ingeliheshimu masharti ya mkataba husika.

Mheshimiwa Spika, hoja yenyewe ni hoja namba 5.1.2.6 inayohusiana na uwepo wa deni la muda mrefu linalodaiwa kwa Kampuni ya Bima Mtawanyo ya UAP Tsh. 564,882,415 na Shirika la Meli la Zanzibar Tsh. 344,275,825.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi nyengine zilizopata hoja kutokana na maagizo ya Serikali ni baadhi ya Serikali za Mitaa ambazo zina kianzio cha mapato ya minara baada ya Serikali kuagiza mapato hayo kukusanywa na Kampuni ya Al - jumura.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa suala hili nimeshalielezea kabla kwenye taarifa yangu ya mapato na matumizi naomba maelezo hayo yatoshe kuwa ni ufafanuzi wa suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mdhibiti, hivyo, imezibakisha hoja hizo kama ilivyo na inapendekeza kwa Serikali kuachana na tabia ya kuzilazimisha Taasisi zake kutekeleza mambo ambayo hayaendani na malengo na dhamira ya kuanzishwa kwa Taasisi husika kwani kuendelea kufanya hivyo kunazitia hasara Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati ya LAAC inashauri hivyo, kwa kuwa zipo baadhi ya Taasisi kama vile Shirika la Bima ambalo kwa mujibu wa majukumu yake huongozwa pia na masharti mengine yaani Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania "TIRA".

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ya LAAC inaitahadharisha Serikali kupitia agizo lake ililolitoa kwa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) la kuwataka kutoendelea kulikodisha jengo lake la Kinazini kwa Watu Binafsi na badala yake jengo hilo likodishwe kwa Taasisi za Umma tu, Taasisi ambazo kwa asilimia kubwa kuna muonekano wa kutokulipa kodi hiyo jambo linaloweza kuibua hoja kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haikuridhishwa na agizo hilo la Serikali kwani jengo hilo linatumiwa na Shirika kama ni kianzio chake cha mapato, hivyo, kuwekewa masharti ya nani wa kukodishwa haileti sura nzuri kwa maendeleo ya Shirika hili.

**Mheshimiwa Spika,** tayari baadhi ya Taasisi za Serikali zimeshahamia ikiwemo, Wizara ya Biashara na Mandeleo ya Viwanda, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kadhalika.

### 4. Baadhi ya Viongozi wa Serikali kuingilia utendaji wa Taasisi za Umma

**Mheshimiwa Spika,** mara kadhaa Kamati ya LAAC imekuwa ikibaini kuwa baadhi ya Viongozi wa Serikali huingilia utendaji wa Taasisi za Umma jambo ambalo huvisa utendaji wa Taasisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imelibaini hili ilivyokuwa inatekeleza jukumu lake huko Shirika la Nyumba ambapo hivi sasa Shirika hili limeanza kuchukua hatua ya kuwatoa ndani ya majengo hayo Wapangishwaji waliovunja mkataba kama vifungu vya 33 na 34 cha Sheria Namba 6 ya mwaka 2014 vinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hatua hiyo inayochukuliwa na Shirika, baadhi ya Wapangaji wa nyumba hukimbilia kwa Viongozi wa Serikali na Viongozi hao wamekuwa wakitoa amri mbali mbali kwa Watendaji wa Shirika hili kwa lengo la kuwalinda Wapangaji hao.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha Viongozi hao kutoa amri hizo kinaviza juhudi za Watendaji wa Shirika hilo na kulikosesha Shirika mapato ambayo ndio chanzo kikuu cha Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 16 Novemba, 2022 Kamati ya LAAC wakati inatekeleza shughuli zake katika Shirika la Nyumba - Pemba ilipokea taarifa kuwa tarehe 14 Novemba, 2022 Mtendaji wa Shirika hilo kwa upande wa Pemba amepigwa na mwananchi wa kawaida wakati anatekeleza majukumu yake kitendo kilichopelekea Mtendaji huyo kushindwa kuhudhuria kazini kwa muda wa siku mbili mfululizo kutokana na maumivu makali aliyoyapata.

**Mheshimiwa Spika,** ili kasoro kama hizo zisijotokeza tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Viongozi wa Serikali wasiwabughudhi Watendaji wa Shirika la Nyumba endapo wanatekeleza majukumu yao kisheria.
2. Viongozi wa Serikali kusimamia kwa dhati mapato ya Serikali na wasiwe chanzo cha kuzuia mapato hayo kwa kuzingatia kuwa Shirika la Nyumba linamilikiwa kwa asilimia mia moja na Serikali, lakini pia, Shirika hilo lina kazi kubwa ya kukarabati nyumba za maendeleo na ujenzi wa nyumba mpya katika maeneo mbali mbali Zanzibar.
3. Vyombo vinavyohusika na ulinzi na usalama vitoe mashirikiano kwa Shirika hili wakati wa zoezi la kuwatoa katika majengo Wapangishwaji waliovunja mkataba ili kuepusha kutokea vitendo viovu dhidi ya Watendaji wa Shirika.
4. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vihakikishe kuwa vinawachukulia hatua wananchi wote waliohusika na kitendo kiovu cha kumjeruhi Mtendaji wa Shirika la Nyumba, tarehe 14 Novemba, 2022 alivyokuwa akitekeleza wajibu wake ili iwe fundisho kwa wengine na hasa ikizingatiwa kuwa hadi tunawasilisha taarifa hii hakuna mtu yeyote aliyekamatwa dhidi ya kitendo hicho .

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa Shirika la Biashara la Taifa haijiamulii mambo yake yenyewe hususan kwenye masuala ya bei ya karafuu na badala yake bei hiyo hupangwa na Serikali jambo linalopelekea karafuu hizo kuuzwa chini ya bei ya soko na hatimae Shirika hili kupata hasara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imehisi ni vyema ikalisema hili kwa kuwa iliwahi kutokea kwa Shirika hili kukosa hata fedha za kuwalipa mishahara Watendaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haipingani sana na maamuzi hayo ya Serikali, isipokuwa kwamba, inaishauri Serikali kuilipia tofauti inayojitokeza kama inavyofanya kwa suala la mafuta, umeme, na kadhalika ili Shirika lisiendelee kupata hasara.

5. **Kuwekwa masharti mahsusi katika vifungu vya Sheria na Kanuni ili kila Taasisi ya Umma iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya masharti ya Sheria na Kanuni zilizopo yanakwaza utendaji wa baadhi ya Taasisi na endapo Taasisi hizo zinazokwazika zikitoa ushauri juu ya jambo husika basi hujibiwa na Serikali majibu ambayo yanakatisha tamaa kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika,** mfano mzuri wa jambo hilo ni kwa Shirika la Bima la Zanzibar kuendelea kutumia Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 kwa hapa nitagusia zaidi kwenye eneo la uondoshaji wa mali za Shirika zilizokuwepo Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima limepata hoja namba 5.1.2.9 kuhusiana na uwepo wa matumizi ya gharama kubwa za maegesho ya masalia ya magari kwani utaratibu wa uuzaji na uondoaji wa mali za Serikali uko chini ya Mamlaka ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango halijachukua hatua ya kuziondosha mali hizo, hivyo, Shirika limekuwa likihifdhi masalia hayo katika karakana ya mtu binafsi ili kuepuka hasara ya uharibifu kwa kuwa Shirika halina eneo la kuweka masalia hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika liliiomba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuliruhusu kumtumia Mtia Thamani wa Shirika ambaye amethibitishwa ili masalia hayo yauzwe kwa haraka na kuepuka gharama zaidi, hata hivyo, Ofisi hii ililijibu Shirika hili kufuata taratibu na miongozo inayotolewa na Ofisi hiyo kwani Shirika la Bima linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haipingani na maamuzi hayo ya Serikali, isipokuwa kwamba, inawaomba watendaji kutumia lugha laini wakati wanavyowasiliana ili kila mtendaji ajione kuwa ana thamani katika Serikali yake.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu kwa kuwa Sheria ya Ununuzi iliyopo hivi sasa inaelekeza

hivyo. Hata hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Taasisi inayohusika na Sheria ya Ununuzi kuifanyia marekebisho Sheria hiyo kwa kuwa masharti yaliyowekwa utekelezaji wake unakwaza baadhi ya Taasisi. Hivyo, ni busara ikatungwa Sheria ambayo masharti yake yataziwezesha Taasisi kuitekeleza Sheria hiyo kwa mujibu wa majukumu yao.

**6. Kutokuwepo kwa hesabu ya matumizi ya kawaida**

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imezitaka baadhi ya Taasisi za Pemba kufungua hesabu ya matumizi ya kawaida. Taasisi zenyewe ni Shirila la Magazeti kufuatia hoja namba 5.2.3.6 na Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) kufuatia hoja namba 5.4.2.7

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC katika kufuatilia hoja hiyo ilitofautiana na ushauri wa Mdhibiti kwa kuwa matumizi ya Taasisi hizo sio makubwa, hivyo, kufungua hesabu ya matumizi ni kuzitia hasara zisizo na msingi Taasisi hizo kwa kuwa zitalazimika pia kuajiri baadhi ya Watendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC ilipendekeza kwa Shirila la Magazeti na Mamlaka ya Usafiri Baharini kutumia njia ya hundi “cheque” au “Telegraphic Transfer” – (T.T) kwa matumizi ya Afisi ya Pemba badala ya kufungua hesabu ya matumizi ya kawaida.

**7. Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kuwasilisha Taarifa yake kwa Mdhibiti**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa asilimia kubwa ya Taasisi za Umma haziwasilishi taarifa za Kamati ya Ukaguzi wa Ndani (Audit Committee) kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama kanuni ya 149(2)(n) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC inazishauri Taasisi zote za Umma kuwasilisha taarifa hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwa Afisi hii ina majukumu mawili ya kitaifa kama jina la Afisi hiyo linavyosomeka.

**8. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akimaliza ukaguzi wake awasilishe nakala ya barua kwa Afisa Mas’uul**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC katika kutekeleza shughuli zake imebaini kuwa baadhi ya taarifa zilizotolewa na Afisi za Pemba zina mapungufu kwa kuwa baadhi ya mambo taarifa zake zipo Makao Makuu ya Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inamuomba Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kumaliza ukaguzi wake kumpatia nakala ya barua inayoonesha hoja za awali za Taasisi husika "Management letter" Afisa Masuul wa Taasisi hiyo ili aweze kujua kasoro zilizopo ndani ya Taasisi yake pamoja na kutoa mashirikiano ya kujibu hoja hizo kwani Afisa Masuul hao walisikitishwa na baadhi ya majibu yaliyotolewa na Taasisi zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inashauri hilo kwa kuwa wakati inatekeleza shughuli zake ilibaini utofauti wa taarifa zilizopo Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na taarifa zilizopo Afisi za Pemba kwa jambo moja.

**9. Utofauti wa kiuandishi baina ya barua ya maombi ya fedha na hati ya malipo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya hoja hujitokeza kutokana na tofauti ya kiuandishi baina ya barua ya maombi ya fedha na hati ya malipo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hilo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Umma kuwa makini zinapoandaa taarifa zake mbali mbali ili kuwa na kauli moja kwa kile kitu ambacho kinaombwa kwa lengo la kuepuka hoja zisizo na msingi.

**10. Changamoto ya Rasilimali Watu katika Taasisi za Umma**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa asilimia kubwa ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinakabiliwa na uhaba wa Watendaji jambo linalopelekea baadhi ya Taasisi zake kushindwa kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa leo naomba niitolee mfano Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ambapo Serikali ilijitahidi kujenga Vyuo vya Mafunzo ya Amali ili kuwapatia ujuzi mbali mbali wananchi wake kwa lengo la kujiari kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kuwaajiri watu wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa bado Vyuo hivyo havina wataalamu wa kutosha wa kutoa kila fani inayohitajika. Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuipa kipaombele Mamlaka hii juu ya suala la ajira kwani Mamlaka inahitaji kwa ujumla watendaji 500, isipokuwa kwamba, kwa kuanzia iliomba nafasi 92 na ikaruhusiwa kuajiri watendaji 20 tu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalisisitiza hili kwa kuwa ilifanya ziara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji – Pemba, hata hivyo, Kamati haikuridhika na mazingira yaliyopo katika Chuo hicho kwa kuwa Serikali imetumia gharama nyingi ya kujenga majengo ya Chuo na hatimae tija inayopatikana ni ndogo.

**11. Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka kinyume na taratibu za Kitaifa na Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imebaini kuwa asilimia kubwa ya Wahasibu

hufunga hesabu za mwisho wa mwaka kinyume na utaratibu, ingawa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huzifanyia marekebisho taarifa hizo lakini bado zinakuwa na makosa makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mapungufu yaliyobainika katika Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka "Financial Statement" kwa Taasisi mbali mbali na Kamati ni pamoja na:

1. Ufafanuzi wa kihasibu (Note) moja kuwa na zaidi ya matumizi ya aina moja;
2. Baadhi ya "Note" kutokuwa na ufafanuzi;
3. "Note" moja kuwa na zaidi ya kiwango kimoja cha fedha, na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuwapatia mafunzo Wahasibu wake wote ili kuwa na ufahamu wa pamoja juu ya uandishi wa Taarifa hiyo, lakini pia, taarifa hiyo hutumika kama ni muongozo katika kupima taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi husika kwani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hutoa Hati za ukaguzi kwa mujibu wa Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

### 12. Serikali kuendelea kuzitaka Taasisi zake kutumia mfumo wa "Cash basis"

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imesikitishwa na kitendo cha Serikali cha kuendelea kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis", jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mashirika kwa mujibu wa viwango vya kihasibu (Financial Accounting Standards) vilivyopo Kitaifa na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalisema tena suala hili kwa kuwa Serikali bado haijaona hasara inayopatikana endapo Taasisi itatumia mfumo huo. Mheshimiwa Spika, Taasisi kutumia mfumo wa "Cash Basis" kunapelekea baadhi ya taarifa muhimu kutoonekana, taarifa ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa Shirika husika kifaida au hasara pamoja na kutojulikana kwa madeni yanayodaiwa na yanayodai Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mfumo huo una mapungufu yake, Kamati ya LAAC inaitaka Serikali kuziruhusu Taasisi zake kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kutumia Mfumo wa "Accrual Basis", mfumo ambao unajumuisha taarifa zote zikiwemo za uchakavu wa mali na uwezo sahihi wa kifedha wa Taasisi ambao hutoa taarifa halisi na sahihi "true and fair view".

### 13. Kamati ya LAAC kutokupata muda wa kutosha wa kufuatilia zoezi la ulipaji wa fidia kwa Waathirika waliopisha ujenzi wa Bandari ya Mafuta na Gesi Mangapwani

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufuatilia hoja hii kama ilivyoelezwa katika Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi Wakati wa Kuwaapisha Viongozi

Wakuu, Kamati ya LAAC ilifanya majadiliano na Waathirika mbali mbali na ililalamikiwa kuwa yapo baadhi ya mapungufu kwa mfano:

1. Baadhi ya Waathirika ambao wanahaki ya kulipwa fidia hawakupewa fedha zao,
2. Baadhi ya Waathirika ambao hawakupokea fedha zao kwa madai kuwa fedha hizo ni kidogo kuna taarifa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili yao ziliingizwa kwenye hesabu ya benki na zimeshatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati yako kupokea malalamiko hayo kutoka kwa Waathirika, Kamati hii haikupata muda wa kutosha wa kufuatilia suala hili, hivyo, inaliomba Baraza lako Tukufu kuridhia kuteua baadhi ya Wajumbe kutoka Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati na Kamati ya LAAC kufuatilia kwa kina suala hili ili haki itendeke.

**Mheshimiwa Spika,** tunapendekeza kazi hiyo ifanyike nje ya siku za Kamati ili Wajumbe wapate muda wa kutosha wa kufuatilia hili pamoja na kuweza kujakushiriki kikamilifu katika kazi zao za Kamati.

**14. Kamati ya LAAC kutokuridhika na Ujenzi wa Nyumba za Wanakijiji Gongoni Zilizojengwa na Vikosi vya SMZ**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haikuridhika na Ujenzi wa Nyumba za Wanakijiji Gongoni waliopisha ujenzi wa Bandari ya Mafuta na Gesi Mangapwani. Nyumba hizo zilizojengwa na Vikosi vya SMZ baada ya kutakiwa na Serikali kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haikuridhika na ujenzi wa nyumba hizo kutokana na baadhi ya sababu zifuatazo:

1. Nyumba hizo zilijengwa kwa gharama kati ya Tsh. 53,000,000 hadi Tsh. 43,000,000 gharama ambazo hazikuwa na uhalisia kwa mujibu wa nyumba husika, kitendo kilichopelekea kutopatikana ufanisi uliotarajiwa katika ujenzi wa nyumba hizo. Hii ni kutokana na kuwa Wajenzi wa nyumba hizo (Vikosi vya SMZ) walipendekeza nyumba hizo kujengwa kwa gharama zifuatavyo ambazo Serikali ilihisi ni gharama kubwa:

    a. Makisio ya awali ya ujenzi wa nyumba hizo walipendekeza kujengwa kwa gharama ya Tsh. 120,000,000, isipokuwa kwamba, gharama hizo zilionekana kuwa ni kubwa sana na Serikali aliwataka wapunguze.
    b. Makisio ya pili wakapendekeza Tsh. 93,000,000 ambazo pia zilionekana gharama hizo kuwa ni kubwa.
    c. Makisio ya tatu wakapendekeza Tsh. 75, 000,000 nazo zikaonekana kuwa ni nyingi.

2. Baadhi ya karo za nyumba hizo zipo juu wakati nyumba zipo chini jambo linalopelekea uchafu kushindwa kutiririka vizuri na hivyo, karo hizo huziba.
3. Karo 1 kutumiwa na jumla ya nyumba 8 kitu ambacho ni kinyume na taratibu za kiujenzi.
4. Masafa ya zilizopo karo na nyumba ni marefu sana, hivyo, uchafu hushindwa kutiririka vizuri na hatimae karo huziba kila baada ya muda mfupi na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kasoro nyingi zilizoibuliwa, Kamati ya LAAC ilifanya mahojiano na Wajenzi wa nyumba hizo na waliieleza Kamati kuwa walikuwa wanatoa ushauri juu ya mambo mbali mbali, isipokuwa kwamba, ushauri wao ulikuwa hausikilizwi na Mshauri Elekezi ambae ni Wakala wa Majengo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchunguzi huo, Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Serikali kuwa na utaratibu wa kuwasilikiza Wataalamu wake na sio kufanya kazi kwa mazoea.
2. Kwa kuwa Taasisi inayolipa gharama juu ya jambo husika ndio inayokaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na dosari yoyote itakayobainika inabebwa na Taasisi hiyo, hivyo, Taasisi hiyo ipewe nafasi kubwa ya kusimamia na kutoa ushauri katika jambo husika na isibakie kama Mtazamaji tu.

   **Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa katika ujenzi huu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) ilikuwa haina fursa ya kufuatilia au kuhoji chochote, isipokuwa kwamba, kazi yao ilikuwa ni kutoa vifaa tu.

3. Kasoro zote zilizobainika kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo kabla ya athiri kubwa kutokea na kuitia hasara Serikali.

## 3.1 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba nimalizie mukhtasari huu kwa kutamka kwamba, Kamati ya LAAC imeziunga mkono kwa asilimia kubwa hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alizozibaini. Hata hivyo, Kamati ya LAAC pamoja na kuunga mkono kwake huko imeridhika na baadhi ya jitihada zilizochukuliwa na Serikali mara baada ya hoja hizo kubainika na hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Ofisi ya Mkaguzi Mkuu kuzifuta hoja hizo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nifanye tathmini ndogo ya kazi tuliyoifanya kwa zile Taasisi

tulizobahatika kuzifanyia kazi kipindi hiki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Serikali za Mitaa, Kamati ya LAAC haikuridhika na utendaji wa Baraza la Mji Mkoani na Baraza la Manispaa Mjini katika mwaka wa fedha 2019/2020 na kwa upande wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea Kamati ya LAAC haikuridhika na utendaji wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kwa Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya LAAC inaziomba tena Taasisi za Serikali kuipa mashirikiano ya dhati Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale inapotekeleza jukumu lake na wasiione Ofisi hiyo kama adui kwao pamoja na kufanya maandalizi mara tu wanapopokea barua ya mwaliko wa Mkaguzi katika Taasisi zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalisisitiza hili kwa kuwa Baraza la Mji Chake chake lilishindwa kumpatia vielelezo vyenye thamani ya Tsh. 32,388,860 Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa madai kuwa vielelezo hivyo vilikuwa vinafanyiwa kazi na Mkaguzi wa Hesabu za Ndani wa Wizara husika aliyekuwepo afisini hapo kwa ajili ya kufanya ukaguzi maalum wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati ya LAAC inalisisitiza hili kwa kuwa baadhi ya hoja huandikwa na Mkaguzi Mkuu baada ya kukosa maelezo ya kina kwa wahusika, isipokuwa kwamba, inapokwenda Kamati hupata maelezo ya kujitosheleza na endapo Kamati itawauliza Watendaji kwa nini majibu kama hayo wasimpatie Mkaguzi basi Watendaji hao huwa hawana majibu.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Taasisi iliyopata hoja kutokana na kushindwa kujieleza ni Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ambayo ilidaiwa kufanya matumizi yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa, Tsh. 27,591,790. Hata hivyo, kutokana na maelezo yao Kamati ya LAAC iliridhika na majibu hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuipatia fedha za matumizi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa wakati ili Ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa Ofisi hiyo ilikaribia kushindwa kuwapatia uchambuzi wa Ripoti zake za mwaka wa fedha 2020/2021 Wajumbe wa Kamati hizo kutokana na uhaba wa fedha unaoukabili Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** ni matarajio ya Kamati hii kuwa Serikali itazifanyia kazi kasoro zote zilizobainika na Kamati pamoja na kuyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza na ninawaomba waijadili na hatimae kuipitisha Ripoti ya Kamati ya LAAC kwa lengo la kutekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** NAOMBA KUTOA HOJA.

……………………

**Mwanaasha Khamis Juma,**

Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti

Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashiriki,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**